www.xtrapapers.com

M15/2/ANSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili ab initio – Standard level – Paper 1
# Swahili ab initio – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili ab initio – Nivel medio – Prueba 1

Friday 8 May 2015 (afternoon)
Vendredi 8 mai 2015 (après-midi)
Viernes 8 de mayo de 2015 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

2215 – 2835



© International Baccalaureate Organization 2015

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

www.xtrapapers.com



**Matini A**

# Mabadiliko ya Mazingira

Kutokana na uchunguzi wa hivi majuzi, hali ya anga imebadilika kwa kuwa na joto jingi zaidi ya kiwango cha kawaida. Hali hii ni jambo ambalo linawafanya wanasayansi kutoka ulimwenguni kote kuungana pamoja na kuanza kutafuta suluhu ya janga hili.

Mojawapo ya sababu za joto jingi angani ni moshi wenye gesi za kemikali hatari kutoka viwandani. Moshi huu huweza kuyeyusha hozoni ambayo ni mwavuli wa miale yenye nyuzi za juu zaidi kufika ardhini. Inapoyeyushwa miale ile hufika ardhini moja kwa moja pasipo pingamizi lolote.

Swala lingine nyeti ni lile la ukataji miti ovyoovyo. Jambo hili linasababisha kuenea kwa jangwa. Hatimaye ardhi iliyokuwa na rotuba huchimbika na kuwa kavu na yenye mabonde yasiyolimika. Haya yote hatimaye huleta ukosefu wa chakula.

Suluhu kuu ni kuwahamasisha watu wote kuhusu kuyatunza mazingira na uwajibikaji katika kuboresha mandhari yetu. Ni wajibu wa kila mmoja kuhusika katika kuhifadhi mazingira.



High Flyer Publishers, *High Flyer Series* (2013)

www.xtrapapers.com



**Matini B**

# Habari za Wakulima

## Kilimo cha Kahawa nchini Congo

Katika kituo cha ukulima cha Kashenda, kamati saba za wakulima wa kahawa zimeundwa. Kilimo cha kahawa huko Kashenda ndio muhimu zaidi kuliko kilimo kingine chochote kile. Kilimo cha kahawa kina faida zaidi kuliko mazao mengine.

Kahawa inayolimwa ndani ya kituo cha kashenda imepandwa na wakulima wenyewe. Wakulima hawa walipanda kahawa hii kufuatana na bei nzuri ya kahawa iliyokuwepo. Kwa sasa, wakulima wa kahawa wameanza kuregea kwa sababu soko la kahawa limeenda chini.

Hata hivyo kuna matumaini ya soko la kahawa kukua kutokana na mafunzo ya mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu kujitegemea na kutafuta masoko mazuri ulimwenguni. Hii ndio maana wakulima wa Kashenda wataungana na wale wa kituo cha Minova ili kutafuta pamoja soko zuri.

Kwa hivyo wakulima wa Kashenda na wale wa Minova watatambuliwa kwa kukazia kazi hizo za kahawa. Wakulima hawa wanahimizwa wasikate tamaa ila watengeneze mashamba yao vyema kwani kahawa ni mojawapo ya mazao ambayo huhitajika nchini na hata ulimwenguni kote.

Sharti wote wafahamu kwamba kwa sasa migomba imesumbuliwa na magonjwa kwa hivyo ni muhimu kutilia mkazo kilimo cha kahawa ili waweze kujipatia pato.

Hamuli Constanin, *Wakulima Amkeni* (2008)

www.xtrapapers.com



**Matini C**

## Mazungumzo ya Babu na Mjukuu wake

*Katana anayeishi mtaa wa Kisauni amemtembelea babu yake huko mtaa wa Nyali mjini Mombasa.*



**Katana**: Shikamoo Babu?

**Babu**: Marahabaa mjukuu wangu. U hali gani?

**Katana:** Salama Babu. Mbona siku hizi umeadimika sana?

**Babu**: Ni maradhi madogo madogo yameniweka ndani ya nyumba, mjukuu wangu. Nimeugua ugonjwa wa malaria lakini sasa nimehisi nafuu.

**Katana:** Lakini babu, huu ugonjwa wa malaria unasababishwa na nini?

**Babu:** Mjukuu wangu, wanasayansi wanasema kwamba ugonjwa huu unasababishwa na mbu hasa wakati huu wa mvua nyingi.

Maji yaliyosimama huwa ni mazingira mwafaka ya mbu kuzaliwa na kuukua haraka sana. Iwapo watu hawatajikinga kwa kutumia neti wakati wanapolala, basi huvamia damu zao.

**Katana:** Sikujua Babu unaelewa sayansi namna hiyo!

**Babu:** Kwa kiasi kidogo mjukuu. Lazima mtu aelewe mambo haya ndio aweze kujikinga. Isitoshe, mbu pia hukaa mahali kwenye nyasi nyingi. Hii ndio sababu niliagizia mtwana wa ami wako aje afyeke nyasi hapa kwangu. Hii ndio njia ya kimsingi ya kujiweka salama.

**Katana**: Hewala, asante babu kwa kunielezea haya. Hata mimi yatanifaa na nitahakikisha mazingira ya nyumbani kwetu ni salama. Upate afueni kwa haraka. Habari za nyanya je?

**Babu**: Ni njema. Yeye ni buheri wa afya. Leo alienda sokoni kuninunulia matunda. Vipi nyumbani jamii inaendeleaje?

**Katana**: Wote ni wazima, wanakukosa sana. Wamenituma nifikishe salamu zao kwenu. Binamu yangu Yusuf hajambo?

www.xtrapapers.com



**Babu:** Hana neno. Siku hizi amekuwa mrefu sana. Siku zinaenda kasi mno na vijana kukua haraka. Hivi sasa ameenda kununua mkate na maziwa ili apike chai ya saa kumi. Punde si punde atarudi.

[Baada ya muda mfupi, Yusuf anawasili akibeba kikapu chenye mkate na maziwa na anajiunga na mazungumzo.]

**Yusuf**: Habari za mchana Katana?

**Katana**: Njema sana Yusuf. Upo?

**Yusuf:** Nipo bwanamdogo binamu. Habari za nyumbani kwenu?

**Katana**: Ni nzuri, watu hawana neno. Leo nimewatembelea japo kwa muda mfupi.

**Yusuf:** Sadakta. Nalisukuma gurudumu la maisha. Tayari niko mwaka wa pili katika masomo yangu ya Diploma. Hivi karibuni, yaani mwezi wa tano, nitafanya mtihani wangu wa mwisho katika kiwango hiki. Maisha hapa kwa babu ni mazuri sana.

**Katana**: Hongera binamu. Nakutakia ufanisi katika masomo yako.

[Akimgeukia babu yake.]

Babu, mimi sasa ninaondoka. Nyanya akirudi mwambie nitarejea nyakati za likizo.

**Babu**: Asante sana mjukuu wangu kwa kuja kutusalimia. Nimefurahi sana na nyanyako akisikia habari zako atafurahi sana.

**Katana**: Shukrani babu. Hata mimi nimefurahi kukuona.

**Babu**: Safiri vyema mjukuu wangu. Kwaheri ya kuonana. Wasalimie wote.

**Katana:** Asante babu.

Yusuf Mdawida, William Andayi na Mathias Momanyi, *Kurunzi ya Marejeleo Halahala, Kiswahili* (2009)

www.xtrapapers.com



**Matini D**

# Usafiri Tanzania

**NDEGE:** Kuna mashirika ya ndege machache ya Tanzania kama ATC na Precision Air. Ndege zinaruka kutoka Dar es Salaam mpaka Arusha, Mwanza, Dodoma, Tanga na miji mingine. Kwa kuwa mashirika ya ndege ni machache, mara nyingine safari zinafutwa.




Ndege

**MELI:** Zipo meli na boti zinazosafirisha abiria katika bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Katika bahari ya Hindi, meli huanzia safari zake katika bahari ya Dar es Salaam hadi Mtwara, Tanga, Zanzibar, Pemba pamoja na kisiwa cha Mafia.



Meli



Treni

**RELI**: Zipo njia mbili za reli ambazo ni Reli ya Kati na Reli ya TAZARA. Treni ya Reli ya Kati inaanzia safari zake kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma, Mwanza na Moshi. Reli ya TAZARA pia huanzia Dar es Salaam na kuishia New Kapiri Mposhi nchini Zambia.



Basi

www.xtrapapers.com



**BARABARA**: Kuna usafiri mwingi wa magari. Watu wengi husafiri kwa mabasi, malori na magari madogo. Kuna mabasi mengi yanayosafirisha abiria kutoka Dar es Salaam hadi Moshi, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Songea, Tanga na kadhalika.



Lori

**KWA MGUU:** Watanzania wengi hasa vijijini wanatembea kilomita nyingi wanapokuwa safarini, wanapokwenda shambani, wanapokwenda kuvua samaki, kuwinda, wanapokwenda kuchota maji, wanapokwenda kukata kuni, wanapokwenda hospitali au zahanati.



Kwa mguu

Kiswahili na Utamaduni Ltd, *Swahili Book for Beginners* (2011)